

KINYWA NA MENO WILAYANI NGARA

Utangulizi

Huduma za afya ya kinywa na meno Wilayani Ngara zilianza rasmi mwezi machi mwaka 2008 na kwa wakati huo idara ilikuwa na mtaalam mmoja tu aliyeanza kazi kwa kutumia kiti cha kawaida cha ofisini (Office chair) baada ya kukosekana kwa kiti maalum cha kutolea huduma(Dental chair) na vifaa vya huduma vichache kwa wakati huo. Baadaye wilaya iliweza kupata kiti maalum na baadhi ya vifaa vya msingi kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia wakati huu idara imefanikiwa kuwa na vifaa vya msingi karibu vyote vinavyotakiwa kutolea huduma kwenye ngazi ya Wilaya na ina jumla ya wataalamu wawili tu baada ya mmoja kufukuzwa kazi kwa masuala ya kinidhamu. Pamoja na watumishi wawili waliopo serikalini idara pia inatoa huduma kupitia wataalam wawili waliopo kwenye hospitali za makanisa (Rulenge na Murgwanza), wastani wa wagonjwa 3000 huonwa kila mwaka katika idara hii kupitia vituo vyake mbalimbali.

Vituo vinavyotoa huduma

Hadi wakati huu vituo vinavyotoa huduma ya afya ya kinywa na meno hapa wilayani ni pamoja na-:

- Hospitali ya Nyamiaga
- Hospitali ya Rulenge
- Hospitali ya Murgwanza
- Kituo cha Afya Bukiriro
- Zahanati binafsi ya Kabanga
- Kituo cha afya Tumaini na
- Kituo cha afya Mabawe

Huduma zitolewazo na idara

Idara kwa ujumla wake inatoa huduma mbalimbali za kinywa na meno kadiri ya miongozo iliyopo, huduma hizo ni pamoja na -:

- Huduma ya kung'oa meno na urekebishaji wa taya zilizofyatuka
- Huduma ya kuziba meno
- Huduma ya kusafisha meno
- Huduma ya matibabu ya mivunjiko
- Huduma ya matibabu ya majipu ya mdomoni(Ukamuaji wa majipu)
- Huduma ya ukataji wa Vinyama vilivyoota mdomoni(Flap excision)
- Huduma ya utoaji wa elimu ya afya ya kinywa na meno

Mafanikio

Katika kipindi cha miaka kumi ya uhai wake, idara ya afya ya kinywa na meno Wilayani Ngara imepata mafanikio yafuatayo-:

- Idara imefanikiwa kupata vifaa karibu vyote vya msingi vya kutolea huduma
- Idadi ya watumishi imeongezeka kwa nyakati tofauti toka mtumishi mmoja hadi wanne
- Idara imeweza kutoa mafunzo ya utoaji huduma za dharula za magonjwa ya kinywa na meno kwa watoa huduma wapatao kumi.
- Idara imefanikiwa kuanzisha utoaji wa huduma wa masaa 24
- Idara imefanikiwa kuanzisha vituo viwili vya kutolea huduma za dharula za kinywa na meno

- Kwa mwaka huu idara imefanikiwa kutoa huduma ya elimu na uchunguzi wa kinywa na meno kwa wanafunzi takribani 500 wa shule za msingi Ngara mjini, Mubinyange na Murgwanza.

Changamoto

Pamoja na mafanikio yote hayo yaliyotajwa, idara ina kabiliwa na changamoto kadha wa kadha. Changamoto hizo ni pamoja na -:

- Kukosekana kwa dawa za kutolea huduma kwa nyakati tofautitofauti
- Watumishi wawili kuondoka kazini kwa sababu mbalimbali
- Uhaba wa wataalamu wa afya ya kinywa na meno unaosababisha vituo vya afya kukosa huduma stahiki
- Kukosekana kwa daktari wa kinywa na meno mwenye stahhada(Dental Surgeon)
- Ufinyu wa bajeti ya ununuzi wa vifaa vya kutolea huduma unaosababisha watumishi waliofanya mafunzo ya utoaji wa huduma za dharula kushindwa kuanza kufanya kazi kwenye maeneo yao.

Mikakati ya kuboresha huduma

- Kuendelea kuwasiliana na ofisi ya Mkurugenzi kupitia ofisi ya Mganga Mkuu juu ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuimarisha huduma za idara
- Kuendelea kuwasiliana na ofisi ya utumishi juu ya kuomba nafasi kwa ajili ya wataalamu wa afya ya kinywa na meno
- Kuwashawishi wataalam wa afya ya kinywa na meno kuja kufanya kazi wilayani Ngara.
- Kutenga bajeti kwa ajili ya kutoa elimu ya afya ya kinywa na meno mashuleni.